

Est

Chapter 6

Swahili Interlinear

Reference: Swahili Biblica Neno

סֵפֶר	אֶת־	לְהַבִּיאַ	וַיֹּאמֶר	הַמֶּלֶךְ	שָׁנַת	נִדְרָה	הָהוּא	בַּלַּיְלָה	1
kitabū	-	kuletwa	na-akasema	wa-mfalme	usingizi	ilimkimbia	ule	usiku	
	H0853	H0935	H0559	H4428	H8142	H5074	H1931	H3915	
	הַמֶּלֶךְ:	לְפָנַי	נִקְרָאִים	וַיְהִי	הַיָּמִים	דְּבָרַי	הַזְּכָרֹנֹת		
	mfalme	mbele-ya	yakisomwa	na-yakawa	ya-siku	mambo	cha-kumbukumbu		
	H4428	H6440	H7121	H1961	H3117	H1697	H2146		

Usiku ule mfalme hakupata usingizi, hivyo akaagiza aletewe kitabu cha kumbukumbu za matukio ya utawala wake, asomewe.

שְׁנֵי	וְתֵרֶשׁ	בִּגְתָנָא	עַל־	מֹרְדֵכַי	הַגִּיד	אֲשֶׁר	כָּתוּב	וַיִּמְצָא	2
wawili	na-Tereshi	Bigthana	kuhusu	Mordekai	aliripoti	kwamba	imeandikwa	na-ilionekana	
H8147	H8657	H0904		H4782	H5046		H3789	H4672	
בַּמֶּלֶךְ	יָד	לְשֵׁלַח	בְּקִשׁוֹ	אֲשֶׁר	הַסֵּף	מִשְׁמָרַי	הַמֶּלֶךְ	סְרִישִׁי	
juu-ya	mkono	kuweka	walitafuta	ambao	wa-mlango	walinzi	wa-mfalme	matowashi	
H4428	H3027	H7971	H1245			H8104	H4428	H5631	
								אַחַשְׁוֵרוֹשׁ:	
								mfalme	
								H0325	

Kitabu hicho kilikutwa na kumbukumbu kwamba Mordekai alikuwa amefichua jinsi Bigthana na Tereshi, waliokuwa maafisa wawili wa mfalme, walinzi wa lango walivyokuwa wamepanga hila ya kumuua Mfalme Ahasuero.

זֶה	עַל־	לְמֹרְדֵכַי	וַגְדוּלָהּ	יָקָר	נִעֲשֶׂה	מָה־	הַמֶּלֶךְ	וַיֹּאמֶר	3
hii	juu-ya	kwa-Mordekai	na-ukuu	ya-heshima	ilifanywa	nini	mfalme	na-akasema	
H2088		H4782	H1420	H3366		H4100	H4428	H0559	
דְּבָרַי:	עִמּוֹ	נִעֲשֶׂה	לֹא־	מִשְׁרָתִי	הַמֶּלֶךְ	נִעְרִי	וַיֹּאמְרוּ		
jambo	kitu	pamoja-naye	hakufanywa	waliomhudumia	wa-mfalme	vijana	na-wakasema		
H1697			H3808	H8334	H4428	H5288	H0559		

Mfalme akauliza, "Je, ni heshima na shukrani gani Mordekai alipokea kwa ajili ya jambo hili?" Watumishi wake wakajibu, "Hakuna lolote alilofanyiwa."

	הַמֶּלֶךְ	בֵּית־	לְחֻצָּר	כָּא	וְהָמָן	בְּחֻצָּר	מִי	הַמֶּלֶךְ	וַיֹּאמֶר	4
	wa-nje	ua	kwa	alikuja	na-Hamani	katika-ua	ni-nani	mfalme	na-akasema	
	H4428			H0935	H2001		H4310	H4428	H0559	
אֲשֶׁר־	הָעֵץ	עַל־	מֹרְדֵכַי	אֶת־	לְתֹלוֹת	לְמִלְךְ	לְאֹמֶר	הַחֵיצוֹנָה		
mti	juu-ya	Mordekai	-	kumtundika	kwa-mfalme	kusema	ya-mfalme	wa-nyumba		
	H6086		H4782	H0853	H8518	H4428	H0559	H2435		
								לִי:	הַכִּין	
								aliandaa	ambao	

Mfalme akasema, "Ni nani yuko uani?" Wakati huo huo Hamani alikuwa ameingia ua wa nje wa jumba la mfalme kusema na mfalme kuhusu kumwangika Mordekai katika mahali pa kuangikia watu alipokuwa amepajenga kwa ajili yake.

5 וַיֵּאמְרוּ נַעֲרֵי הַמֶּלֶךְ אֵלָיו הֲנָה הַמֶּן עִמָּךְ בְּחֹצֵר
na-wakasema vijana wa-mfalme kwake angalia Hamani amesimama katika-ua
[H0559](#) [H5288](#) [H4428](#) [H0413](#) [H2009](#) [H2001](#) [H5975](#)

וַיֵּאמֶר הַמֶּלֶךְ יָבוֹא: na-akasema mfalme aingie
[H0559](#) [H4428](#) [H0935](#)

Watumishi wake wakamjibu, "Hamani amesimama uani." Mfalme akaamuru, "Mleteni ndani."

6 וַיְבֹאֵם הַמֶּן הַמֶּלֶךְ וַיֵּאמֶר לֹא הַמֶּלֶךְ מֵהֵרָ לַעֲשׂוֹת בְּאִישׁ אֲשֶׁר
na-akaingia Hamani na-akasema kwake mfalme nini kufanya kwa-mtu ambaye
[H0935](#) [H2001](#) [H0559](#) [H4428](#) [H4100](#) [H0376](#)

הַמֶּלֶךְ הַפֶּן בִּיקְרוּ וַיֵּאמֶר הַמֶּן הַמֶּלֶךְ לְמִי יִחַפֵּן
mfalme anapenda kumheshimu na-akasema Hamani kufanya kwa-nani atapenda
[H4428](#) [H3366](#) [H0559](#) [H2001](#) [H4428](#) [H4310](#)

הַמֶּלֶךְ לַעֲשׂוֹת יָקָר יוֹתֵר מִמֶּנִּי: mfalme kufanya heshima zaidi kuliko-mimi
[H4428](#) [H3366](#) [H3148](#)

Hamani alipoingia, mfalme alimuuliza, "Afanyiwe nini mtu ambaye mfalme apenda kumheshimu?" Basi Hamani akawaza moyoni mwake, "Ni nani mwingine ambaye mfalme angemheshimu kuliko mimi?"

7 וַיֵּאמֶר הַמֶּן אֶל- הַמֶּלֶךְ אִישׁ אֲשֶׁר הַמֶּלֶךְ הַפֶּן בִּיקְרוּ:
na-akasema Hamani kwa mfalme ambaye mfalme anapenda kumheshimu
[H0559](#) [H2001](#) [H0413](#) [H4428](#) [H0376](#) [H4428](#) [H3366](#)

Kwa hiyo akamjibu mfalme, "Kwa mtu ambaye mfalme apenda kumheshimu,

8 וַיְבִיאֵם לְבוֹשׁ מַלְכוּת אֲשֶׁר לְבָשׁ- בּוֹ הַמֶּלֶךְ וְסוֹס אֲשֶׁר רָכַב
waleta vazi la-kifalme ambalo amevaa balo mfalme na-farasi ambaye amempanda
[H0935](#) [H3830](#) [H4438](#) [H3847](#) [H4428](#) [H7392](#)

עָלָיו הַמֶּלֶךְ וְאֲשֶׁר נָתַן כֶּתֶר מַלְכוּת בְּרֵאשׁוֹ: mfalme na-ambaye imewekwa taji ya-kifalme kichwani-mwake
[H4428](#) [H5414](#) [H3804](#) [H4438](#)

aletewe joho la kifalme ambalo mfalme ameshalivaa na farasi ambaye mfalme alishampanda, ambaye amevikwa taji ya kifalme kichwani mwake.

9 וַנִּתּוֹן הַלְבוּשׁ וְהַסּוֹס עַל- יָד- אִישׁ מִשָּׁרֵי הַמֶּלֶךְ הַפְּרָתָיִם
na-kutoa vazi na-farasi kwa mkono wa-mtu kutoka-wakuu wa-mfalme wakuu
[H5414](#) [H3830](#) [H3027](#) [H0376](#) [H8269](#) [H4428](#) [H6579](#)

וְהַלְבִּישׁוּ אֶת- הָאִישׁ אֲשֶׁר הַמֶּלֶךְ הַפֶּן בִּיקְרוּ וְהִרְכִּיבֵהוּ עַל-
na-wamvike - mtu ambaye mfalme anapenda kumheshimu na-wamtembeze juu-ya
[H3847](#) [H0853](#) [H0376](#) [H4428](#) [H3366](#) [H7392](#)

הַסּוֹס בְּרִחְבּוֹ הָעִיר וְקָרְאוּ לְפָנָיו כִּכָּה יַעֲשֶׂה לְאִישׁ
farasi katika-barabara ya-mji na-wapige-kelele mbele-yake hivyo itafanywa kwa-mtu
[H7339](#) [H7121](#) [H6440](#) [H3602](#) [H0376](#)

אֲשֶׁר הַמֶּלֶךְ הַפֶּן בִּיקְרוּ: mfalme anapenda kumheshimu ambaye
[H4428](#) [H3366](#)

Kisha joho na farasi vikabidhiwe kwa mmojawapo wa wakuu wa mfalme anayeheshimika sana. Nao wamvike mtu yule ambaye mfalme anapenda kumheshimu, na aongozwe akiwa juu ya farasi kupitia barabara za mji, wakitangaza mbele yake, 'Hivi ndivyo anavyofanyiwa mtu ambaye mfalme apenda kumheshimu!'"

כְּאִשֶׁר	הַסּוֹס	וְאֶת־	הַלְבִּיֹשׁ	אֶת־	חֻקָּה	מֵהָרַר	לְהַמָּן	הַמְלִיךְ	וַיֹּאמֶר
kama-vile	farasi	na-	vazi	-	chukua	haraka	kwa-Hamani	mfalme	na-akasema
		H0853	H3830	H0853	H3947		H2001	H4428	H0559
הַמְלִיךְ	בְּשַׁעַר	תֵּיּוֹשֵׁב		תֵּיּהוּדִי	לְמֹרְדֵכַי	כֵּן	וַעֲשֵׂה־	דִּבְרֹתָ	
pa-mfalme	langoni	ambaye-anaketi		Myahudi	kwa-Mordekai	hivyo	na-ufanye	ulivyosema	
H4428	H8179	H3427		H3064	H4782			H1696	
				דִּבְרֹתָ:	אֲשֶׁר	מִכֹּל	דָּבָר	תַּפִּל	אֶל־
				umesema	ulichosema	kila	kutoka	neneno	usipunguze
				H1696		H3605	H1697	H5307	H0408

Mfalme akamwamuru Hamani, "Nenda mara moja, chukua joho na farasi na ufanye kama vile ulivyopendekeza kwa Mordekai Myahudi, akaaye langoni mwa mfalme. Usipuuze kufanya kitu chochote ulichoshauri."

מֹרְדֵכַי	אֶת־	וַיִּלְבָּשׁ	הַסּוֹס	וְאֶת־	הַלְבִּיֹשׁ	הַמָּן	וַיִּקַּח	
Mordekai	-	na-akamvika	farasi	na-	vazi	-	Hamani	na-akachukua
H4782	H0853	H3847		H0853	H3830	H0853	H2001	H3947
וַעֲשֵׂה	כְּכֹה	לְפָנָיו	וַיִּקְרָא	הָעִיר	בְּרָחוֹב	וַיִּרְכִּיבֵהוּ		
itafanywa	hivyo	mbele-yake	na-akapiga-kelele	ya-mji	katika-barabara	na-akamtembeza		
	H3602	H6440	H7121		H7339	H7392		
			בִּיקְרוֹ:	חָפִיץ	הַמְלִיךְ	אֲשֶׁר	לְאִישׁ	
			kumheshimu	anapenda	mfalme	ambaye	kwa-mtu	
			H3366		H4428		H0376	

Hivyo Hamani akachukua joho na farasi. Akamvika Mordekai, na kumpandisha juu ya farasi akamtembeza katika barabara za mji akitangaza mbele yake, "Hivi ndivyo anavyofanyiwa mtu ambaye mfalme anapenda kumheshimu!"

בֵּיתוֹ	אֶל־	נִדְחָה	וְהַמָּן	הַמְלִיךְ	שַׁעַר	אֶל־	מֹרְדֵכַי	וַיֵּשֶׁב
nyumba-yake	kwa	aliharakisha	na-Hamani	la-mfalme	lango	kwa	Mordekai	na-akarudi
	H0413	H1765	H2001	H4428	H8179	H0413	H4782	H7725
					רֹאשׁ:	וְחַפּוּי	אָבֵל	
					kichwa	na-amefunika	akiomboleza	
						H2645	H0057	

Baadaye Mordekai akarudi kwenye lango la mfalme. Lakini Hamani akakimbia nyumbani, akiwa amejaa huzuni,

כָּל־	אֵת	אֲהָבָיו	וּלְכָל־	אֲשֶׁתּוֹ	לְזֶרֶשׁ	הַמָּן	וַיֹּסִיפֶר	
kila	-	wote	na-kwa-wapenzi-wake	mke-wake	kwa-Zereshi	Hamani	na-akawaambia	
H3605	H0853	H0157	H3605	H0802	H2238	H2001		
אִם	אֲשֶׁהוּ	וְזֶרֶשׁ	חֻקָּיו	לוֹ	וַיֹּאמְרוּ	קָרְהוּ	אֲשֶׁר	
kutoka	ikiwa	mke-wake	na-Zereshi	wenye-hekima-wake	kwake	na-wakasema	kilichompata	
	H0802	H2238	H2450		H0559			
תּוֹכַל	לֹא־	לְפָנָיו	לְנַפְלִי	תַּחֲלוֹת	אֲשֶׁר	מֹרְדֵכַי	תֵּיּהוּדִים	מִנְרַע
kwake	hutamshinda	mbele-yake	kuanguka	umeanza	ambaye	Mordekai	wa-Wayahudi	uzao
H3201	H3808	H6440	H5307			H4782	H3064	H2233
			לְפָנָיו:	תַּפּוּל	נַפּוּל	כִּי־	לוֹ	
			mbele-yake	mbele-yake	utaanguka	kuanguka	bali	
			H6440	H5307	H5307			

naye akamweleza Zereshi mkewe pamoja na rafiki zake wote kila kitu ambacho kimempata. Washauri wake pamoja na Zereshi mkewe wakamwambia, "Kwa kuwa Mordekai, ambaye mbele yake umeanza kuanguka ni wa asili ya Kiyahudi, huwezi kushindana naye; kwa hakika utaanguka!"

וַיִּבְהֹלוּ	הִגִּיעוּ	הַמְלִיךְ	וְסָרִיסֵי	עָמֹד	מְדַבְּרִים	עוֹדֵם	14
walifika	wa-mfalme	na-matowashi	pamoja-naye	wanasema	bado	wao	
H0926	H5060	H4428	H5631		H1696	H5750	
אֶסְתֵּר:	עֲשֵׂתָהּ	אֲשֶׁר-	הַמְשִׁתָּהּ	אֶל-	הַמֶּן	אֶת-	לְהַבִּיא
alifanya	ambayo	karamu	kwa	Hamani	-	kuleta	na-wakaharakisha
H0635			H4960	H0413	H2001	H0853	H0935

Walipokuwa bado wakizungumza naye, matowashi wa mfalme wakaja na kumharakisha Hamani aende katika karamu aliyoiandaa Esta.